

**Swahili transcript:**

Upendo: Kwa nini labda waigizaji wa filamu wa Tanzania wanapenda ku-copy kutoka katika filamu za ki-Nigeria? Labda nini kilichowapelekea wao kuweza ku-copy aah! Vile vitu ambavyo wanaviona katika filamu za ki-Nigeria?

Happy: Mimi nadhani kwanza ni uvivu; uvivu wa kufikiria. Kwa sababu kama wakifikiria, kuna filamu nyingine ambazo tunazona wanazo wanazozitoa kwa sasa hivi ziko tofauti. Ni watu wachache ambao wanatengeneza filamu ambazo ziko tofauti na zile za ki-Nigeria. Ila wale ambao wanapenda ku-copy kutoka kwa wa-Nigeria ni kutokana na uvivu. Hawataki kufikirisha vichwa vyao na kuja na kitu ambacho ni sasa hiki ni cha kwetu, hiki ni pekee, hiki ni kweli cha kitanzania. Kwa hiyo, mimi nadhani wasanii wengi wa Tanzania wanatakiwa waache uvivu. Halafu pia elimu. Wengi wa wasanii sidhani kama wana elimu ya kiasi kikubwa ya kiasi hicho; yaani kwamba wakae wakifikiria kwa nini tuna-copy kutoka kwa wa-Nigeria? Kwa nini tusije na kitu ambacho ni cha kwetu sisi wenyewe watanzania? Kwa hiyo nadhani pia elimu ina...yaani changamoto kubwa ni kwamba wasanii wanatakiwa wapate elimu ili waweze kufikiria zaidi na pia waondokane na uvivu.

Upendo: Au pia labda unafikiri aah! Yawezekana pia filamu za ki-Nigeria labda zina mvuto zaaidi ndio maana watanzania wameona wa-copy kutoka kwa wa-Nigeria ?

Happy: Aaah! Kwa kweli mimi sidhani kama zina mvuto, sijui. Mimi si mpenzi sana wa filamu za ki-Nigeria, lakini kwa kweli katika filamu nyingi ambazo nimeshaona mpaka hapa, nyingi zina mambo ya kutisha. Ni chache sana ambazo zinakuwa tu zina stori ya kawaida, au zinachekesha; kwa mfano zile za kina Akwi na Ukwa (kicheko) ambazo utacheka. Lakini yaani nyingi, nyingi ya filamu za ki-Nigeria zina mambo ya kutisha ; ambayo kwangu mimi, kwa kweli hapana ; siwezi kuangalia, zinaniogopesha. Lakini kuna filamu nyingine nzuri, kwa mfano zinazoelezea kuhusu story au vichekesho. Na pia sio watanzania wote ambao wanatengeneza filamu hizo za kutisha, lakini nyingi zao ukiona kwa mfano sijui msyuka, sijui damu imefanya nini ; yaani unaona filamu inavyokuwa inatangazwa kwenye TV

Upendo: Unaogopa

Happy: Mpaka mwenyewe unakuwa hupati hata ile hamu ya, ladha ya kwenda kusema sasa hii filamu imetoka nikanunue, maana kila kitu ni damu tu. Mara sijui huyu katokea shetani, sijui.

Upendo: Na suala jingine labda aah! Waigizaji wa kitanzania, waigizaji wa filamu kwamba mara nyingi wanazitoa filamu katika muda mfupi, yaani ni muda mfupi filamu inatoka, muda mfupi filamu inatoka. Je, unaweza ukaniambia hiyo inasababishwa na nini

labda? Nini kinachowafanya labda watoe filamu katika muda mfupi mfupi maana utakuta filamu nyingine nimeziona zinakuwa hazina ubora, hazina kiwango kizuri, labda ni kutokana wameenda katika muda mfupi. Sasa je labda ni kitu gani kinachowapelekea wakatoa filamu katika muda mfupi mfupi na badala ya kukaa labda katika muda mrefu na kufikiria nini tufanye filamu itoke ikiwa nzuri, wao wanatoa filamu katika muda mfupi?

Happy: Kwa kweli hapo sina jibu sahihi sana, labda mimi nadhani wanataka hela (kicheko) Ukitoa filamu uka..ukaiuza,watu wakanunua ukapata hela, basi

Upendo: Na una changamoto gani sasa kwa waigizaji filamu wa kitanzania?

Happy: Aaah! Mimi napenda tu kuwaambia wajitahidi, waweze kujiendeleza. Kwa mfano hapo walipofikia sio kwamba ndio mwisho. Watu wanajitahidi, wanajiendeleza ili kuweza kupata soko kubwa zaidi. Na pia waache uvivu wa ku-copy copy, wajitahidi kuja na vitu vipya, idea mpya ambazo wao wenyewe zitakuwa zinaonyesha maisha halisi ya watanzania, na sio kama ambavyo wata-copy kutoka katika nchi nyingine ambazo tunaona wanatengeneza filamu.

Upendo: Asante kwa maelezo yako mazuri.

Happy: Asante Upendo.

### **English translation:**

Upendo: What makes Tanzanian filmmakers copy Nigerian films?

Happy: The first reason is laziness. Tanzanians don't devote much time to thinking about what they want to do; that's why they copy other films. There are some films which are good. You can tell that they sit down and think about it and come up with the real thing, truly Tanzanian, but these are very few and they are different from other films. Actors should stop being lazy so that they can produce good films which reflect the Tanzanian culture, and not another country's culture. Another issue is that many actors don't have enough education about the film industry. They need to be educated and when they make films, they will come out with something good because it will come from their own ideas. The big challenge to Tanzanian actors is education, and another thing is, they need to stop being lazy.

Upendo: Maybe Nigerian films attract people and that's why Tanzanians copy from them?

Happy: I don't think so. First of all, I am not a lover of Nigerian movies. Most of the Nigerian films I have watched so far are frightening. Very few of them have stories or comedies like Akwi and Ukwa (laughter). Most of the Nigerian films are distressing and I don't want to watch something which upsets my life. Not all Tanzanians make violent

films, but you can see threatening scenes in television ads for films like *Msyuka*, where you see bloodshed. The ad keeps me from wanting to watch such a movie.

Upendo: Tanzanian actors have been making movies for a short period of time. What makes them do so? I have seen some of the films which have been released recently, and they are not good quality films. I think it's because they didn't take the time to think and produce something good. What do you think led them to doing so?

Happy: I don't have the right answer, but what I think is that they want money, (laughter), that's it. When you make a film and sell it and people buy tickets, you get money, that's it.

Upendo: What challenges do you have for Tanzanian film actors?

Happy: I believe that education will help them succeed in their field. They need education so that when they make films. Their films will have good quality and many people will love to buy and watch their movies. Then the film market will increase. They should also stop copying from Nigerians. They should come up with new ideas that reflect the real life of Tanzanians.

Upendo: Thanks for your good explanations.

Happy: Thanks Upendo.

**About CultureTalk:** CultureTalk is produced by the Five College Center for the Study of World Languages and housed on the LangMedia Website. The project provides students of language and culture with samples of people talking about their lives in the languages they use everyday. The participants in CultureTalk interviews and discussions are of many different ages and walks of life. They are free to express themselves as they wish. The ideas and opinions presented here are those of the participants. Inclusion in CultureTalk does not represent endorsement of these ideas or opinions by the Five College Center for the Study of World Languages, Five Colleges, Incorporated, or any of its member institutions: Amherst College, Hampshire College, Mount Holyoke College, Smith College and the University of Massachusetts at Amherst.

© 2003-2008 Five College Center for the Study of World Languages and Five Colleges, Incorporated